# Kwa nini mara nyingine uume hausimami?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ili mwanaume aweze kujamii ana, ni lazima uume usimame na kuweza kupenya ukeni. Kama mvulana anasisimka kimapenzi, damu nyingi inaenda katika mishipa ya damu ndani ya uume. Halafu uume husimama kutokana na msukumo wa damu. Hivyo kama msukumo wa damu hautoshi, hii husababisha uume kutosimama au kusimama kwa unyonge.

Kutokuwa na msisimko wa kutosha kwa ajili ya kusimamisha uume kunaweza kusababishwa na mambo mengi, mojawapo ni i i ile hali ya kutokuwa tayari kwa kujamii ana, kuwa na wasiwasi mwingi, kutompenda mpenzi wako, ulevi wa pombe au dawa za kulevya, kuvuta sigara, lishe duni au maradhi mbalimbali. Kama una shida ya uume kutosimama wakati wa kujamii ana, jaribu kuangalia ni sababu zipi kati ya hizi zilizoorodheshwa juu zingeweza kuwa sababu kuu ya shida yako. Halafu, jaribu kurekebisha matatizo.